JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MADINI**

Telegramu " MADINI"
Simu: +255- 26-2320456
Barua Pepe:ps@madini.go.tz

Mji wa Serikali- Mtumba
S. L. P.422,
**41207 DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

# TANZANIA MLANGO WA AFRIKA MASHARIKI KATIKA FURSA ZA UWEKEZAJI WA MADINI MKAKATI NA MUHIMU

**Dar Es Salaam, Tarehe 23 Mei 2023**

Kwenye uzinduzi rasmi wa Kongamano la Uwekezaji katika Sekta ya Madini Mwaka 2023 linalojulikana kama ***Tanzania Mining & Investment Forum 2023***, litakalofanyika tarehe 25- 26 Oktoba 2023, **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini** alizungumza kuhusu fursa za kipekee zilizopo nchini Tanzania kwenye Sekta ya Madini.

Alisema, “Kwa heshima na taadhima ninayo furaha kubwa kuwakaribisha kwenye mkutano huu wa Uwekezaji kwenye sekta ya madini na pia naomba nichukue fursa hii kuwakaribisha wageni wote waalikwa katika uzinduzi wa leo. Naomba kutumia fursa hii kuwakaribisha wadau wote waliopo kwenye sekta ya madini nchini Tanzania, bara la Afrika na ulimwenguni kote, kushiriki Kongamano la Madini na Uwekezaji litakalofanyika Dar Es Salaam tarehe 25 na 26 Mwezi Oktoba mwaka wa 2023. Lengo la mkutano huu; ni pamoja na kuwasilisha taarifa muhimu za sekta ya madini, kuwa na vikao vya mazungumzo na wawekezaji, kubainisha fursa zilizopo kwenye miradi ya madini, na kuimarisha ushirikiano wa ndani na nje ya nchi katika kukuza na kuifanya sekta ya madini Tanzania kuwa endelevu. Nawakaribisha sana Tanzania kwani kwa sasa ni miongoni mwa nchi zenye mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.”

Tanzania ni moja kati ya nchi zilizopo Afrika Mashariki, ambayo inakisiwa kuwa ni kitovu cha uzalishaji na uendelezaji wa madini mkakati na muhimu yanayotumika kutengeneza vifaa vitakavyosaidia matumizi ya nishati safi. Tanzania inavutia wawekezaji mbalimbali kutoka ulimwenguni kote kutokana na uwepo wa utajiri wa madini ya aina mbalimbali, sera rafiki na ongezeko kubwa na uhitaji wa nishati endelevu.

Tanzania imebarikiwa kuwa na madini mkakati na muhimu yanayohitajika katika uzalishaji wa magari ya umeme, miundombinu ya nishati mbadala, na tekinolojia nyingine zinazozalisha nishati safi . Miongoni mwa madini mkakati na muhimu yanayopatikana Tanzania ni lithiamu, Kobalti, Nikeli, *Graphite* na madini adimu. Madini hayo yamekuwa na thamani kubwa kutokana na mwelekeo wa kidunia katika uendelezaji wa uchumi unaozingatia uzalishaji mdogo zaidi wa hewa ya ukaa (low carbon economy). Kwa kuzingatia hilo Serikali ya Tanzania hivi karibuni imesaini

mikataba na kampuni tatu za Australia (Evolution Energy Minerals, EcoGraf Ltd na Peak Rare Earths) kwa ajili ya uchimbaji wa madini muhimu ikiwemo graphite. Miradi hiyo yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 667 ni utekelezaji wa mpango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuongeza kasi ya majadiliano kwenye miradi ya muda mrefu kwenye sekta ya madini.

Wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika sekta za nishati safi na madini mkakati na muhimu wanashauriwa kuitazama Tanzania. Mazingira yake mazuri ya uwekezaji pamoja na wingi wa maliasili ni katika vitu vinavyoifanya kuwa kivutio kikubwa cha uwekezaji. Aidha, sehemu ilipo kijiografia kunaifanya Tanzania kuwa mlango mkubwa wa masoko ya Afrika Mashariki.

Serikali ya Tanzania imeweka Sheria na kanuni za kuwezesha njia bora za uchimbaji wa madini kwa ajili ya usalama wa jamii na mazingira zinazoshabihiana na za Kimataifa. Pamoja na haya, Serikali ya Tanzania imeweka kipaumbele suala la Uongezaji thamani na uchakataji wa madini nchini ili kuongeza ajira, mapato na pia kuimarisha biashara miongoni mwa watanzania wenyewe.

Vilevile, Tanzania ni mwanachama wa Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, mafuta na Gesi Asilia (Extractive Industries Transparency Initiative - TEITI) inayozingatia uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa madini na maliasili kwa ujumla. Hatua hii inawapa wawekezaji uhakika kuwa sekta ya madini nchini inasimamiwa kwa umakini wa hali ya juu, uendelevu na yenye kuwajibisha.

**Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko** alihitimisha hotuba yake na Vyombo vya Habari kwa kusema “nawakaribisha kwa dhati wawekezaji wote kuja nchini Tanzania, kitovu cha madini ya Tanzanite na mlango wa fursa katika Afrika Mashariki kwa madini mkakati na muhimu. Asanteni sana kwa kunisikiliza,” .

**MWISHO**

**Kwa maswali yoyote yanayohusiana na nafasi ya kuzungumza, ufadhili, maonesho na usajili wa wahudhuriaji** kwenye Kongamano la Madini na Uwekezaji au biashara Tanzania tafadhali wasiliana na:
Meneja Masoko, Danai Davatzis danaidavatzis@dmgevents.com; +255 755 030 622, au tembelea www.tanzaniamininginvestmentforum.com; au mitandao yetu ya kijamii LinkedIn, Facebook, Twitter, Instagram na utumie #TanzaniaMiningForum kwa habari mpya, taarifa na matangazo ya mara kwa mara kuhusu kongamano.

**Kwa taarifa zaidi juu ya shughuli za dmg na Ocean Business Partners Tanzania Ltd** katika uandaaji wa hafla za kimataifa nchini Tanzania tembelea www.dmgevents.com na www.obp-tanzania.co.tz kujifunza zaidi.

**Kuhusu Kongamano la Madini na Uwekezaji**

Kongamano la Madini na Uwekezaji litawavutia zaidi ya watu 2,000 kutoka nchi zaidi ya 25 ulimwenguni itakayo ambatana na mkutano utakao hodhi zaidi ya wazungumzaji 100, wenye zaidi ya vipindi 20, hotuba za keynote na maonyesho makubwa ya teknolojia na uvumbuzi. Kongamano

la mwaka huu litaweka mazingatio makubwa zaidi kwenye uwekezaji wa kimataifa, uchimbaji wa madini, miradi mipya, ushirikiano, teknolojia na uwezeshaji. Aidha, patakuwa na mada mpya za kujadili mambo ikiwemo sera za Serikali juu ya mazingira, jamii na utawala, mikakati ya maendeleo ya sekta ya madini, uchimbaji wa madini endelevu, pamoja na uzalishaji wa ndani.

**Kuhusu Shughuli za dmg**

**dmg** ni miongoni mwa kampuni kubwa zinazoandaa hafla za kimataifa wakiwa na kumbukumbu ya hafla 84 katika tasnia mbali mbali wakivutia zaidi ya watu 425,000 kuhudhuria hafla hizo. Shughuli zao zinazohusiana na masuala ya nishati na katika hafla kubwa kuwahi kutokea ulimwenguni zikihusisha ADIPEC, Egypt Petroleum Show, World Utilities Congress, pamoja na Global Energy Show. Kujua zaidi tembelea www.dmgevents.com. Bofya hapa kusoma sera yetu ya faragha.

**Kuhusu Ocean Business Partners Tanzania**

Ocean Business Partners Tanzania ni kampuni mwenyeji na kinara yenye kushauri kampuni za kimataifa ikiwa na mazingatio zaidi kwenye ujuzi katika tasnia mbalimbali kama mafuta, gesi, nishati, usafirishaji, ushauri wa kiuwekezaji, ushauri wa kibiashara, ushauri juu ya uwezekano wa kupatikana hasara, ujenzi wa miradi, pamoja na uwezeshaji wa kifedha. Ocean Business Partners Tanzania inajivunia kuwezesha wateja wake mbalimbali kuanzia hatua za awali wakati wa kuanzisha miradi mpaka hatua za utekelezaji na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwenye soko la mafuta, gesi na nishati kwa ujumla. Dhumuni letu ni kuweza kuandaa mipango na mikakati ya kibiashara bora zaidi kwa ajili ya wateja wetu kwa kutumia mikono ya wabobezi wetu katika sekta husika. Tunaamini katika ushirikiano kwenye jitihada za kutafuta suluhisho mbali mbali katika kila zoezi tunalolidiriki kwa ajili ya wateja wetu. Tembelea tovuti yetu www.obp-tanzania.co.tz kujua zaidi.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Madini**